

INTERNATIONAL RESCUE COMMITTEE

# Uwekaji Muktadha katika Juhudi za Kuzuia na Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia

## Maneno Tu au Hali Halisi kwa Mashirika Yanayoongozwa na Wanawake na ya Kutetea Haki za Wanawake katika Miktadha ya Uhisani?

International Rescue Committee | Desemba 2024

# Shukrani

Faiza Husainy aliongoza uandalizi na uandishi wa ripoti hii. Tunatoa shukrani kwa wenzetu wa Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji (IRC) waliounga mkono uandishi wa ripoti hii, wakiwemo Helena Minchew na Mercy Lwambi, pamoja na wale waliochangia pakubwa katika uandalizi na uratibu wa utafiti huu, wakiwemo Jean Gabriel Carvalho, Suzanie Chito, Albert Kadha, Filston Bitaha Mushagalusa, Yves Zabulisire Kacunguye, na Mireille Ngwamba kutoka timu ya nchi ya DRC; Fabiola Gamboa Ross, Dulce Escalante, Shirley Perez, Glendy Cruz, na Samara Massis kutoka timu ya nchi ya Guatemala; Magda Rossmann na Hana Abu Jalboush kutoka timu ya nchi ya Jordan; Inah Kaloga, Patricia Gray, Cornelia Aton, Camille Andre, Amira Taha, Evelyn Vallejo, Rocky Kabeya, na Rosemary Tola Ogunjobi kutoka Kitengo cha Ufundi wa Kuzuia na Kujibu Vurugu.

Tunatambua na kushukuru wateja waliohudhuria Majadiliano ya Vikundi (FGDs) kwa ujasiri wao na uwazi wa kushiriki uzoefu wao. Sauti zao zilikuwa muhimu katika kuimarisha uchambuzi wetu kwa ukweli wa maisha.

Tunatoa shukrani za pekee kwa wahusika muhimu, wakiwemo mashirika ya kitaifa na ya wanawake yanayoongozwa na wanawake, ambao walitumia muda wao, mitazamo yao, na utaalamu wao katika kazi hii. Shukrani maalum kwa Action Femmes Sourdes (AFS), Bon Dieu Dans La Rue (BDR), Dynamique des Femmes Juristes (DFJ), na Ligue pour la Solidarité Congolaise (LSC) nchini DRC; Asociación de Mujeres Río Isquizal (AMRIS), Mujeres Mejorando Vidas (MMV), na VISIBLES nchini Guatemala; na Jerash Ladies Charity, SIGI Solidarity in Global Institute na Family Guidance and Awareness Center (FGAC) nchini Jordan.

Shukrani zetu za dhati pia zinaenda kwa wafadhili na mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali (INGOs) waliotoa maoni yao muhimu wakati wa Mahojiano ya Watoa Taarifa Wakuu (KIIs), yakiboresha matokeo yetu.

Tunawashukuru pia kwa michango yao: Little Fish (muundo wa picha); Kathryn Murphy (uhariri wa maandishi); Estefanía Calderón Potes (tafsiri ya Kifaransa na Kihispania); Forum Tech (tafsiri ya Kiarabu na Kiswahili).

Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji inapenda kuwashukuru Irish Aid kwa msaada wao katika uandalizi wa chapisho hili. Mawazo, maoni, na maoni yaliyoelezwa hapa ni jukumu la Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji pekee na hayaonyeshi sera ya Irish Aid.

Ripoti hii ni ushuhuda wa juhudi za pamoja za watu wengi, na tunatumaini itatoa mchango mkubwa katika kuboresha mipango ya GBV kimataifa.

*Picha ya jalada la mbele imepigwa na* ***Daniel Ssemogerere kwa ajili ya IRC***

*Picha ya jalada la nyuma imepigwa na* ***Maheder Haileselassie***

Irish Aid
Rialtas na hÉireann
Government of Ireland

# Jedwali la Yaliyomo


**04** **Muhtasari**

**06** **Mapendekezo**

**09** **Ufafanuzi wa istalahi muhimu**

**10** **Utangulizi**

**12** **Sehemu ya 1: Uwekaji Muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia**

» Mifano ya uwekaji muktadha katika hali halisi
» Tathmini ya mbinu za sasa za uwekaji muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia
» Mbinu zinazotumiwa na mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake katika kuwekea muktadha miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia
» Mielekeo katika uwekaji muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia
» Kutathimini ufanifu wa uwekaji muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia

**20** **Sehemu ya 2: Ufadhili na ugawaji wa rasilimali**

» Vikwazo vya ufadhili huzuia uwekaji muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia

**22** **Sehemu ya 3: Vizuizi vya uwekaji muktadha**

» Vizuizi vya utamaduni na vya kijamii
» Vizuizi vya ufadhili na rasilimali
» Vizuizi vya ugavi na uendeshaji
» Vizuizi vya mashirika na uratibu

**25** **Sehemu ya 4: Hitimisho**

**27** **Kiambatisho cha 1: Mbinu**

» Uchambuzi wa machapisho
» Mahojiano na watoa taarifa wakuu
» Majadiliano ya vikundi
» Uteuzi wa sampuli na ukusanyaji wa data
» Masuala ya maadili

**29** **Kiambatisho cha 2: Sauti za wateja**

» Kuangazia DRC
» Kuangazia Guatemala
» Kuangazia Yordani




# Muhtasari

**Unyanyasaji wa kijinsia (GBV) ungali suala muhimu duniani; mmoja kati ya kila wanawake watatu duniani ananyanyaswa kimwili au kingono na mpenzi wake.[1] Licha ya kuwepo kwa viwango na kanuni za kimataifa za kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na kauli za kuwekea suala hili kipaumbele katika serikali mbalimbali na mashirika ya uhisani, takwimu hii inadhihirisha changamoto zilizopo katika kushughulikia suala hili lililoenea. Katika majanga ya kibinadamu, hatari ya unyanyasaji wa kijinsia huongezeka mno.[2] Huku majanga ya kibinadamu yakizidi kuwa makali, ya mara kwa mara na yakidumu kwa muda zaidi, kuna hitaji la juhudi za kudumu na zilizoimarishwa za kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia.**

**Wakati huo huo, mfumo wa uhisani, wakiwemo wafadhili, umesisitiza haja ya "kujanibisha" juhudi za uhisani, pamoja na kuhakikisha kwamba mifumo ya kimataifa inaweza kutumika katika muktadha wa eneo ili kuhakikisha kwamba waathiriwa wanapata usaidizi wa kutosha.**

Licha ya kauli za kusisitiza hayo, uchambuzi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Guatemala na Yordani ulipata kwamba ambapo juhudi za kuweka muktadha haziungwi mkono ipasavyo, vikundi vya wadau mara nyingi hujihusisha katika mzunguko wa kulaumiana, huku vikitambua wenzao kama kiini cha tatizo. Kwa mfano, wafadhili wanaripoti kwamba mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali (INGO) mara nyingi hayatoi usaidizi wa kutosha wa kujenga uwezo kwa washirika wa eneo, hali inayodunisha uwezo wa washirika hao wa kusimamia ufadhili kivyao. Wanaeleza pia kwamba mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali mara nyingi hutaka matokeo yanayolingana na viwango vya kimataifa ambayo huenda hayaendani vyema na muktadha wa eneo. Kwa upande mwingine, mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali yanatoa hoja kwamba wafadhili hawatoi ufadhili kulingana na mahitaji na mara nyingi huwataka washirika wa eneo wawe na uwezo zaidi kabla ya kuweza kusimamia fedha ipasavyo. Mashirika ya eneo nayo yanahisi kutengwa, huku mashirika yanayoongozwa na wanawake (WLO) na mashirika ya kutetea haki za wanawake (WRO) yakitaja kwamba mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali huwawekea mipaka ya kuhusika kwa hofu ya kupoteza udhibiti. Yanaeleza pia kuwa yanatamaushwa na wafadhili kutoitikia mahitaji mahususi ya muktadha wao.

Uchambuzi huo ulipata kwamba kuna changamoto zinazoonekana nzito katika uwekaji hasa wa muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Vizuizi vya kitamaduni na kijamii, kama vile kaida za mfumo dume nchini Guatemala na unyanyapaa wa makazi ya kimbilio nchini Yordani, huwazuia wanawake wengi kupata huduma. Nchini DRC, vikwazo vya ugavi na vya kifedha, ikiwa ni pamoja na usafirishaji

1 https://www.unwomen.org/en/articles/facts-and-figures/facts-and-figures-ending-violence-against-women
2 https://www.rescue.org/article/what-gender-based-violence-and-how-do-we-prevent-it



na miundomsingi duni, huzuia ufikiaji wa huduma muhimu. Isitoshe, utegemeaji wa ufadhili wa muda mfupi na uliowekewa mipaka, pamoja na kutokuwepo kwa ufadhili wa moja kwa moja kwa mashirika ya nchini huzuia uendelevu na upanuzi wa miradi yenye mafanikio.

Katika yote haya, wateja walitaja kwamba changamoto kubwa ni kuwa huduma nyingi hutolewa kwa wateja bila kutambua kwamba unyanyasaji wa kijinsia huathiri na huathiriwa na masuala mengine mengi, hali ambayo mara nyingi huleta madhara yasiyokusudiwa na kufanya wateja wahisi kuwa hawasikilizwi. Ukosefu huu wa juhudi za pamoja unaweza kudunisha huduma zinazozingatia waathiriwa, hasa wakati juhudi zisipozingatia jinsi unyanyasaji wa kijinsia unavyofungamana na masuala mengine ya kijamii, kiuchumi na kiafya.

Ripoti hii inatoa mapendekezo kadhaa ya kushughulikia changamoto hizi. Baadhi—kama vile kuongeza ufadhili wa moja kwa moja na huru kwa Mashirika yanayoongozwa na wanawake na ya kutetea haki za wanawake, na kuboresha uratibu na ushirikiano—yamechukuliwa kwa muda mrefu kama njia za kutimiza malengo ya ujanibishaji, kuongeza uwekaji wa kipaumbele kwa suala la unyanyasaji wa kijinsia katika sekta nzima, kutimiza malengo ya usawa wa jinsia na kuondoa ukoloni katika misaada ya kibinadamu. Ijapokuwa yamerudiwa mara nyingi, mapendekezo haya ni muhimu sana na yanafaa pia katika kuhakikisha miradi bora na inayozingatia muktadha.

Mapendekezo mengine ni pamoja na:

» **Imarisha mbinu za maoni shirikishi na ushughulikiaji wa maoni.** Miradi mingi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia ina mbinu za kupata maoni, lakini tatizo ni kuhakikisha kwamba maoni yanafuatwa na vitendo. Mashirika yanayoongozwa na wanawake, mashirika ya kutetea haki za wanawake na wateja hutoa maarifa muhimu, lakini mara nyingi hawaoni mabadiliko halisi kutokana nayo.

» **Jenga uwezo wa eneo kwa ajili ya uendelevu wa kudumu.** Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake ni muhimu sana katika kuweka muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, lakini mara nyingi yanakumbwa na changamoto za rasilimali, mafunzo na uhuru wa kufanya maamuzi. Kujenga uwezo ni muhimu sana katika kuyapa mashirika haya ujuzi wa kuratibu miradi, usimamizi wa fedha, utetezi, uongozi na ushirikishi wa jamii, kuhakikisha upatano na viwango vya kimataifa na uelekevu kwa mahitaji ya eneo. Usaidizi huu utaimarisha uwezo wa mashirika haya wa kushiriki katika utungaji sera na kuweka muktadha katika miradi ili kutimiza mahitaji ya wateja vyema zaidi.

Maarifa haya yanaangazia hitaji la mbinu yenye ufanisi zaidi ya kuweka muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, hasa kuhusiana na ufadhili, utohozi wa kitamaduni na uratibu.

# Mapendekezo

Mapendekezo yanayofuata yanatokana na uchambuzi wa ushahidi uliopatikana kwa ajili ya ripoti hii.

## 1 Ongeza ufadhili wa moja kwa moja na wenye uhuru

Wafadhili wanafaa kuweka kipaumbele katika kutoa ufadhili wa moja kwa moja kwa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake, ili kuhakikisha yana rasilimali za kusimamia miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kivyao na kuiwekea muktadha. Taratibu za ufadhili zinafaa pia kutoa uhuru wakati wa kutekeleza miradi, na hivi kuwezesha mashirika ya eneo kurekebisha miradi yao kulingana na mahitaji yanayobadilika na maoni ya muda halisi kutoka kwa jamii yanazohudumia. Mikataba ya ufadhili wa miaka kadhaa inaweza kuweka uthabiti unaohitajika kwa mashirika kupanga na kupanua miradi endelevu.

## 2 Imarisha uratibu na ushirikiano

Kuimarisha uratibu miongoni mwa wafadhili, mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali, mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake ni muhimu sana katika kuleta upatano kati ya miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na mahitaji ya eneo na kushughulikia vyema mahitaji ya waathiriwa. Wafadhili walisisitiza umuhumi wa kukuza ushirikiano kupitia mbinu jumuifu za uratibu, kama vile mikutano ya mara kwa mara ya vikundi vya mashirika au vya ushauri, ambapo wahusika wa eneo wana kauli ya maana katika taratibu za kufanya maamuzi.

Mfadhili mmoja alitaja,

> ***“Ni muhimu sana kuwataka washirika kuwajibikia kuleta matokeo kwa ushirikiano na wenzao kati eneo, ili kuhakisha upatano na mahitaji ya eneo.”***

Hili linaangazia haja ya mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali kujumuisha mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake katika kupanga na kutekeleza miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, badala ya kuwachukulia kama wafadhiliwa wadogo wasiohusika.

Mwakilishi wa shirika linaloongozwa na wanawake na la kutetea haki za wanawake alisema katika mahojiano:

> ***“Isipokuwa shirika la kimataifa lisilo la serikali linaloongoza ufadhili, ni nadra sana kwetu kukutana na mfadhili. Mara nyingi, kila mtu hudhani kuwa shirika la kimataifa lisilo la serikali ndilo mfadhili, lakini sivyo.”***

Hili linadhihirisha pengo lililopo kati ya mashirika ya eneo na wafadhili, hali ambayo inaweza kudunisha mafanikio ya miradi iliyowekewa muktadha.

Kwa kujenga majukwaa mahususi ya kubadilishana maarifa na kupanga pamoja, wafadhili, mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali na mashirika ya eneo wanaweza kushiriki mbinu bora, kupunguza kurudia miradi sawa na kuimarisha ufaafu wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kwa muktadha. Ushirikiano kama huu huhakikisha kwamba juhudi ni za pamoja na zinazingatia waathiriwa katika ngazi zote za utekelezaji.

## 3

## Imarisha mbinu za maoni shirikishi na ushughulikiaji wa maoni

Ijapokuwa miradi mingi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia ina mbinu za kupata maoni, tatizo ni kuhakikisha kwamba maoni hayakusanywi tu bali pia yanashughulikiwa. Mashirika yanayoongozwa na wanawake, mashirika ya kutetea haki za wanawake na wateja mara nyingi hutoa maarifa muhimu kuhusu changamoto na mahitaji katika muktadha wao, lakini wengi wanaripoti kuwa maoni yao hayazai mabadiliko halisi.

Mwakilishi mmoja wa shirika linaloongozwa na wanawake alisema,

> ***"Maoni hukusanywa, lakini ni nadra sana yanapoleta mabadiliko tunayoweza kuona."***

Pengo hili hudunisha kuaminiana na kudunisha uwezo wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kubadilika ipasavyo kulingana na hali ya eneo.

Mteja mmoja alisisitiza umuhimu wa mtazamo mpana katika kutimiza mahitaji, akitaja waziwazi katika majadiliano ya kikundi kwamba ijapokuwa ni muhumi kuwa na choo karibu, kina faida tu ikiwa kuna chakula cha kutosha cha kuleta sababu ya kukitumia.

Hii inadhihirisha hitaji la dharura la kujumuisha mbinu za kuhakisha usalama wa chakula katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia ili kuhakikisha ustawi na hadhi ya washiriki.

Vivyo hivyo, mshiriki mwingine alisisitiza umuhimu wa kufululiza msaada vyema, akitaja,

> ***"Sabuni kwanza, kisha bafu."***

Kielelezo hiki kinadhihirisha umuhimu wa kuwekea kipaumbele masuala muhimu kama nyenzo za usafi kabla ya kuwekeza katika maboresho mapana ya miundomsingi.

Ili kushughulikia hili, wafadhili na mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali sharti yaweka michakato ya maoni yenye mwelekeo wa vitendo. Mashirika yanayoongozwa na wanawake, mashirika ya kutetea haki za wanawake na wateja wanafaa kupokea mawasiliano dhahiri kuhusu jinsi maoni yao yameathiri maamuzi ya miradi. Taarifa za mara kwa mara na marekebisho dhahiri kutokana na maoni ya jamii yanafaa kujumuishwa katika michakato ya utekelezaji wa miradi.

Vilevile, wafadhili na mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali yanafaa kutenga rasilimali za kuimarisha uwezo wa mashirika yanayoongozwa na wanawake na wa mashirika ya kutetea haki za wanawake wa kukusanya, kuchambua na kuitikia maoni. Hii ni pamoja na mafunzo ya jinsi ya kujumuisha maoni ipasavyo katika usanifu na utekelezaji wa miradi. Wafadhili na mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali yanafaa kuweka mifumo wazi ya uwajibikaji ambayo wanaweza kutumia kudhihirisha jinsi maoni yameelekeza maamuzi yao na utohozi wa miradi.

Kwa kusikiliza maoni kwa makini na kuchukua hatua za makusudi, wadau wanaweza kuhakikisha kwamba miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia inazingatia waathiriwa na pia inabadilika na kuitikia mahitaji ya jamii wanazolenga kuhudumia.

## 4

## Jenga uwezo wa eneo kwa ajili ya uendelevu wa kudumu

Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake wanatimiza wajibu muhimu katika kuwekea muktadha miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, lakini mara nyingi yanakosa rasilimali, mafunzo na uhuru unaohitajika kutekeleza miradi endelevu na yenye mafanikio. Wafadhili wanapaswa kufadhili juhudi za mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali za kuyapa mashirika haya ujuzi na nyenzo zinazohitajika kuongoza miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kwa kujitegemea.

Mfadhili mmoja alisisitiza pengo hili, akisema,

> ***"Haifai kwamba kila mara mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali hutaja kwamba yana washirika wa eneo katika ufadhili mdogo wanaotoa, lakini baada ya miaka, mfadhiliwa mdogo bado hawezi kuomba ufadhili kivyake."***

Maoni haya yadhihirisha umuhimu wa juhudi za kujenga uwezo ambazo ni zaidi ya usaidizi wa muda mfupi wa kiufundi ili kuhimiza ukuaji endelevu na kujitegemea miongoni mwa mashirika ya eneo.

Suala muhimu lilioibuliwa na mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake ni ukosefu wa uwezeshaji na nafasi inayotolewa na mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali. Kama mwakilishi mmoja wa shirika linaloongozwa na wanawake alivyotaja,

> ***"Mashirika ya Kimataifa Yasiyo ya Serikali yana hofu kwamba tutachukua nafasi yao, kwa hivyo hayatupatii nafasi."***

Mtazamo huu unaonyesha mvutano uliopo kati ya mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali na wahusika wa eneo, ambapo huenda mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali yakasita kuruhusu mashirika ya eneo kuchukua nafasi za uongozi kwa hofu ya kupoteza udhibiti.

Vipengele muhimu vya kujengea uwezo ni pamoja na:

- Kuimarisha uwezo wa mashirika yanayoongozwa na wanawake na wa mashirika ya kutetea haki za wanawake kupanga na kusimamia miradi inayopatana na viwango vya kimataifa na pia hali halisi ya eneo
- Kutoa mafunzo ya usimamizi wa fedha ili kuhakikisha uzingatiaji wa matakwa ya wafadhili
- Kukuza ujuzi wa utetezi na uongozi ili kuwezesha ushiriki bora katika mbinu za uratibu na michakato ya utungaji sera.

Isitoshe, kuunga mkono mikakati ya kushirikisha jamii inaweza kukuza uwezo wa mashirika ya eneo wa kukusanya maoni na kurekebisha miradi ili kutimiza mahitaji ya wateja vyema zaidi.

# Ufafanuzi wa istalahi muhimu

Katika ripoti hii, ufafanuzi ufuatao unatumika:

### MASHIRIKA YA KIMATAIFA YASIYO YA SERIKALI (INGO)

Mashirika yasiyolenga faida yanayofanya kazi katika nchi mbalimbali kutoa msaada wa kibinadamu na miradi ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na juhudi za kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Mara nyingi mashirika haya hushirikiana na mashirika ya eneo kutekeleza miradi iliyowekewa muktadha katika maeneo yanayokumbwa na hatari.

### MASHIRIKA YA KUTETEA HAKI ZA WANAWAKE (WRO)

Mashirika yanayozingatia kuendeleza haki za wanawake, ikiwa ni pamoja na ulinzi wao dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia. Mashirika ya kutetea haki za wanawake hutekeleza wajibu muhimu katika kuweka muktadha katika mipango ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kwa kuhakikisha kwamba juhudi zinalingana na mahitaji ya eneo na viwango vya kimataifa.

### MASHIRIKA YANAYOONGOZWA NA WANAWAKE (WLO)

Mashirika yasiyo ya serikali yanayoongozwa na wanawake wanaotetea na kutekeleza miradi ya kushughulikia masuala yanayoathiri wanawae ikiwa ni pamoja na kuzuia na kukabiliana na Dhuluma za Kijinsia. Mashirika haya mara nyingi huwa na uelewa wa kina wa muktadha wa eneo na huwa muhimu sana katika uwekaji muktadha wa miradi.

### MBINU INAYOZINGATIA WAATHIRIWA

Kanuni muhimu katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia inayoweka kipaumbele kwa mahitaji, hadhi na uhuru wa waathiriwa katika upangaji na utoaji wa huduma. Mbinu hii huhakikisha kwamba waathiriwa hawaumizwi tena, na kwamba sauti na chaguo zao ni kiini cha miradi au usaidizi wowote.

### UFADHILI

Rasilimali za kifedha zinazotolewa na wafadhili, Mashirika ya Kimataifa Yasiyo ya Serikali au wahusika wengine ili kusaidia utekelezaji wa mipango ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Ufadhili wa kutosha na endelevu ni muhimu sana katika kuhakikisha mafanikio na uendelevu wa miradi iliyowekewa muktadha.

### UJANIBISHAJI

Kuwezesha wahusika wa ndani ya nchi zilizoathirika kuongoza na kutoa msaada wa kibinadamu. Lengo lake ni kuimarisha uwezo na rasilimali za mashirika ya eneo kwa ajili ya kukabiliana na hali ngumu na kukuza uendelevu wa muda mrefu. Mchakato huu unatambua umihimu wa maarifa ya eneo na uelewa wa utamaduni katika utoaji wa misaada bora na inayofaa utamaduni. Kwa kuwawezesha wahusika wa eneo, ujanibishaji husaidia kuboresha ufaafu, ufanisi na matokeo ya juhudi za uhisani.[4]

Ujanibishaji usichukuliwe kumaanisha kutafsiri na kurekebisha maudhui kwa ajili ya eneo au lugha fulani, kama vile kubadilisha tovuti kutoka Kiingereza hadi Kihispania kwa ajili ya hadhiara ya Amerika ya Kilatini.

### UNYANYASAJI WA KIJINSIA (GBV)

Kitendo chochote cha kudhuru kinachofanyiwa mtu kwa msingi wa jinsia yake, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kimwili, kingono, kihisia na kiuchumi. Unyanyasaji wa kijinsia umejikita katika mwingiliano ambapo hapana usawa wa nguvu, na ubaguzi kwa msingi wa jinsia unaweza kutoka katika hali nyingi, ikiwa ni pamoja na katika familia, jamii na mazingira ya kazi.

### UTOHOZI

Kurekebisha maudhui yaliyopo ili kufaa hadhira au kusudi jipya.

### UWEKAJI MUKTADHA

Mchakato wa, kwa wakati mmoja:

» Kutathmini kwa kiasi kipi vipengele vya mradi wa kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia vinatekelezwa kulingana na *Kiwango cha Chini cha Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia* katika muktadha mahususi

» Kutambua ni Hatua zipi Muhimu na/au ni hatua zipi za ziada zinapaswa kupewa kipaumbele, kuanzishwa, kutoholewa, kudumishwa, kuimarishwa au kuratibiwa vyema zaidi ili kutimiza kiwango cha chini kabisa kinachohitajika katika muktadha mahususi.

Uwekaji muktadha pia unaweza kujumuisha utambuaji wa washirika bora, ikiwa ni pamoja na mashirika ya wanawake, wa kuratibu nao ili kutimiza Kiwango cha Chini kinachohitajika.[3] Hatua hizi huwasaidia wahisani kuelewa mahitaji ya wateja mahususi na kubuni maudhui yanayoambatana na wateja hao.

### VIZUIZI

Vikwazo vinavyokabili mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake katika kuwekea muktadha na kutekeleza miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Hivi ni pamoja na upinzani wa kiutamaduni, vikwazo vya ufadhili na kutolingana kwa vipaumbele vya wafadhili na mahitaji ya eneo. Vizuizi pia hutokana na matatizo ya uratibu, kama vile ukosefu wa ufadhili wa moja kwa moja kwa mashirika ya eneo, na ugumu wa kuhakikisha kwamba wafadhili wa kimataifa wanaelewa muktadha wa eneo. Vilevile, baadhi ya mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yanakumbwa na vizuizi kama vile kufurushwa, matishio ya usalama na ukosefu wa uwezo wa kutosha wa kieneo wa kumiliki kikamilifu miradi iliyowekewa muktadha.

### WAFADHILI

Mashirika au watu binafsi wanaotoa msaada wa kifedha kwa mashirika yanayoongozwa na wanawake, mashirika yanayotetea haki za wanawake na wahusika wengine wanaotekeleza miradi ya kukabiliana na Unyanyasaji wa kijinsia. Wafadhili hutekeleza wajibu muhimu katika kuelekeza upeo, ukubwa na lengo la miradi iliyowekewa muktadha kulingana na vipaumbele vyao vya ufadhili.

3 *https://gbvaor.net/sites/default/files/2021-01/FGMS_Contextualization%20Tool_EN_Final.pdf*
4 *https://civil-protection-humanitarian-aid.ec.europa.eu/what/humanitarian-aid/localisation_en*

# Utangulizi

Juhudi za uhisani za kukabiliana na Unyanyasaji wa kijinsia (GBV) zimeokoa maisha kwa zaidi ya mwongo mmoja. Ripoti hii inachambua kama huduma za uhisani zinazoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia zinapatikana, zinafaa na zina ufanisi kwa watu katika maeneo mahususi. Lengo la ripoti hii ni kupata picha bayana ya jinsi shughuli za uwekaji muktadha hutekelezwa na matokeo yake kwa wateja na jamii. Inachunguza jinsi mashirika yanayoongozwa na wanawake (WLO) na mashirika ya kutetea haki za wanawake (WRO) huweka muktadha katika miongozo ya kimataifa inayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia (GBV) ili kutimiza mahitaji ya maeneo mahususi, kaida za kitamaduni, mifumo ya sheria na jiografia. Vilevile, ripoti hii pia inachunguza kama mashirika haya hupokea ufadhili wa kutosha kwa ajili ya juhudi zao na kama ufadhili unaopatikana unatosha kutekeleza utohozi huu ipasavyo.

Ripoti hii inachunguza jinsi mashirika huweka muktadha katika miongozo ya kimataifa ili kutimiza mahitaji ya maeneo mahususi, kaida za kitamaduni, mifumo ya sheria na hali halisi ya jiografia katika kila eneo. Imetokana na mahojiano na watoa taarifa wakuu kutoka wafadhili, mashirika ya eneo na ya kitaifa yasiyo ya serikali (NGO), mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali (INGO) na uchambuzi wa machapisho yanayopatikana ya kimataifa, na panapohitajika, ya kitaifa na eneo.

Maarifa kutoka majadiliano ya vikundi na wateja—waathiriwa na pia walio katika hatari ya unyanyasaji wa kijinsia—yalitathmini ikiwa wateja wanahudumiwa kwa njia ambayo inazingatia utamaduni na pia inapatana na mahitaji yao, hivyo kukuza mazingira salama kwao ya kupata huduma na usaidizi.

Kila kikundi cha wadau kilitoa taarifa inayosimulia kama juhudi za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia zinawekewa muktadha na jinsi hili linavyofanywa. Matokeo yanatoa maarifa ya jinsi mashirika ya uhisani yanaweza kufikia juhudi za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia ambazo zimewekewa muktadha, kwa pamoja na kila moja kivyake. Kwa mfano, maoni kutoka kwa wateja katika majadiliano ya vikundi yanaonyesha kiwango cha kuhusika kwao katika mchakato wa uwekaji muktadha na jinsi uzoefu wao wa huduma zinazoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia unavyodhihirisha ufanifu wa juhudi hizi zilizowekewa muktadha wa eneo.

Mahojiano na Mashirika ya Kimataifa Yasiyo ya Serikali yanachunguza jinsi mashirika hayo yanavyofafanua na kuweka kipaumbele kwa uwekaji muktadha katika miradi yao ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, hasa kuhusiana na maamuzi ya uchangishaji fedha na ushirikishaji wa wadau wa eneo lao, ikiwa ni pamoja na mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake katika mchakato wa uwekaji muktadha. Wafadhili walitoa maarifa kuhusu vipengele vya uwekaji muktadha wanavyopea kipaumble kwa ajili ya ufadhili na jinsi wanavyotathmini hitaji la kuweka muktadha.

Mbinu zilizotumita kukusanya na kuchambua ushahidi zimeelezwa katika Kiambatisho cha 1.

Viwango vya Chini vya Kukabiliana na Unyanyasaji



Picha imepigwa na **Daniel Ssemogerere kwa ajili ya IRC**

wa Kijinsia[5] vinatoa mwongozo wa juhudi za kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia katika miradi yote ya kibinadamu. Utekelezaji wake unahitaji kuwekewa muktadha kwa uangalifu ili kutimiza mahitaji ya eneo, kaida za kitamaduni, mifumo ya kisheria na jiografia.

Nyenzo ya Kuweka Muktadha katika Viwango vya Chini vya Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia inaangazia kwamba miradi bora ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia inategemea urekebishaji wa juhudi ili zipatane na hali halisi ya eneo bila kudunisha kanuni za kimataifa. Uwekaji muktadha huimarisha ufanisi wa miradi kwa kushughulikia upungufu wa rasilimali, vizuizi vya utamaduni na mahitaji hasa ya waathiriwa, na hivyo kuhakikishwa kwamba huduma zinapatikana na pia zinaleta matokeo bora.

Ushahidi unadokeza kwamba mbinu zinazozingatia muktadha huhimiza ushirikiano na uendelevu, na hivyo kuleta matokeo bora zaidi kwa waathiriwa.[6] Vivyo hivyo, Mwongoza wa IASC wa Kujumuisha Juhudi za Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia katika Shughuli za Uhisani unasisitiza kwamba uwekaji muktadha ni muhimu sana katika kupunguza hatari na kuimarisha uthabiti katika mazingira mbalimbali ya kibinadamu. Mwongozo huo unatetea kuweka muktadha wa eneo katika mifumo ya kimataifa na kukabiliana na upungufu wa rasilimali, vizuizi vya utamaduni na mahitaji hasa ya waathiriwa ili kuboresha ufaafu na upatikanaji wa miradi.[7]

Sera hizi na nyinginezo, ikiwa ni pamoja na za UNHCR[8] na UNICEF,[9] zinadhihirisha kwamba mbinu zilizotoholewa kufaa eneo ni muhimu sana katika kukuza ushirikiano, kuimarisha uendelevu na kuhakikisha matokeo bora kwa waathiriwa. Kwa kupatanisha juhudi na mahitaji hasa ya jamii na kwa kutumia uwezo wa eneo, wadau wanaweza kukuza miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia yenye uelekevu na ufanifu.

Kuelewa desturi zilizopo, kukadiria mbinu zinazotumiwa na mashirika ya eneo na kutathmini ufaafu wa juhudi hizi za uwekaji muktadha ni muhimu sana katika kuelekeza miradi ya baadaye. Sehemu zifuatazo zitachunguza undani wa kuweka muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, zikianza na tathmini ya kina ya desturi na mikakati ya sasa inayotumiwa na mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake. Pia tunachunguza mienendo inayoibuka, changamoto katika utekelezaji na mafunzo muhimu yaliyopatikana ili kutoa picha pana ya changamoto na suluhu katika utayarishaji wa miradi ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia. Uchambuzi huu wa msingi utafuatwa na uchanganuzi wa kina wa vikwazo vya ufadhili na mapendekezo ya kuimarisha ugawaji wa rasilimali, ambayo ni muhimu sana katika kukabiliana na vikwazo vilivyotambuliwa.

5 https://www.unfpa.org/sites/default/files/pub-pdf/19-200_Minimun_Standards_Report_ENGLISH-Nov.FINAL_.pdf
6 https://gbvaor.net/sites/default/files/2021-01/FGMS_Contextualization%20Tool_EN_Final.pdf
7 https://wrd.unwomen.org/sites/default/files/2021-11/GBV-Implementation-Strategy-Guide-2015_0.pdf
8 https://www.unhcr.org/media/unhcr-policy-prevention-risk-mitigation-and-response-gender-based-violence-2020
9 aa9276_82ef51da8eea4a05906f185d5b977a50.pdf



1

SEHEMU YA 1

# Uwekaji Muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia

Kuweka muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia huhakikisha kwamba inazingatia viwango na kanuni zilizowekwa za kimataifa huku ikitoholewa ili kuendana na hali halisi za kipekee katika miktadha ya eneo. Mchakato huu huzingatia kaida za kitamaduni, mifumo ya kisheria, mahitaji ya jamii na jiografia ya eneo ambapo mradi unatekelezwa. Badala ya kubadilisha viwango vya kimataifa, uwekaji muktadha huzingatia kutekeleza viwango hivi kwa njia zinazofaa, zinazotendeka na zenye matokeo bora katika mazingira ya maeneo mbalimbali. Ushirikiano na mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake ni mhuimu sana, kwa maana mashirika haya huleta uelewa wa kina wa hali halisi ya eneo na kuhakikisha kwamba miradi inaambatana na jamii yanayohudumia.

Uwekaji muktadha huhakikishwa kwamba miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia inazingatia waathiriwa na inapatana na changamoto za kipekee za kila eneo. Unahimiza:

» Ufaafu wa kitamaduni, kwa kudhihirisha desturi na imani za kitamaduni za jamii huku ukihoji kaida zenye madhara

» Kuridhia kwa jamii, kwani miradi iliyowekewa muktadha ina uwezekano mkubwa zaidi wa kupata imani na kuungwa mkono na jamii za eneo, na hivyo kukuza ushiriki na matokeo

» Usaidizi mpana wa waathiriwa, ambapo waathiriwa wanaweza kupata huduma zinazotimiza mahitaji yao ya kijamii, kisaikolojia na kisheria kwa njia inayozingatia utamaduni.

# MIFANO YA UWEKAJI MUKTADHA KATIKA HALI HALISI

Ufuatao ni muhtasari wa desturi za uwekaji muktadha huko DRC, Guatemala na Yordani. Maelezo ya kina zaidi yanapatikana katika Kiambatisho cha 2.



**JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO**

Uwekaji muktadha katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ni pamoja na kujumuisha miradi ya kutoa misaada ya riziki na huduma zinazoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia ili kukabiliana na hatari za kiuchumi zinazozidisha matishio kwa waathiriwa. Kwa mfano, kuwapa wateja mafunzo ya utengenezaji sabuni, ushonaji au utengenezaji wa makaa hakuwapatii njia ya kuchuma mapato tu, bali pia hupunguza utegemeaji wao wa mbinu zenye madhara za kukabiliana na hali yao, kama vile ngono ya kujikimu. Katika maeneo yenye miundomsingi duni, miradi hii huendeshwa katika maeneo yanayofaa jamii ili kuhakikisha yanafikiwa kwa urahisi na ni salama. Mbinu hii ya uwili inashughulikia mahitaji ya sasa ya wateja na masuala ya kimfumo yanayoendeleza hatari ya unyanyasaji wa kijinsia.



**GUATEMALA**

Nchini Guatemala, uwekaji muktadha unazingatia kuwafikia wanawake wa Asili, wengi ambao wanakabiliwa na vikwazo zaidi, kama vile tofauti za lugha na viwango vya chini vya uwezo wa kusoma na kuandika. Kwa kutasfiri nyenzo katika lugha za Kiasili, kama vile Mam au K'iche' (Quiché) na kutumia vielelezo vya kuonekana au usimuliaji, miradi hufanya taarifa muhimu zinazohusu unyanyasaji wa kijinsia zipatikane kwa wote. Vilevile, juhudi za kujenga mahusiano zinalingana na mapendeleo ya jamii, kama vile kufanya mikutano katika maeneo ya jamii yanayoaminiwa au kujumuisha huduma za utunzaji wa watoto ili kuhimiza wanawake wenye majukumu ya kulea washiriki.



**YORDANI**

Nchini Yordani, ambapo makazi ya hifadhi ya wateja mara nyingi hukumbwa na unyanyapaa wa kitamaduni, uwekaji muktadha unajumuisha kubuni njia mbadala za kutoa huduma. Kwa mfano, huduma tamba zinazoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia huwawezesha wateja kupata usaidizi kwa fargha, huku maeneo salama katika vituo vya jamii hutoa mazingira ya kuaminika na yanayokubalika kitamaduni. Juhudi za kuhusisha jamii pia huweka kipaumbele katika kushirikiana na wanaume na wavulana ili kukanusha kaida zenye madhara na kukuza usawa wa jinsia, hatua muhimu katika kuhimiza mabadiliko ya muda mrefu ya kijamii katika mazingira yanayoshikilia ukale.

# TATHMINI YA MBINU ZA SASA ZA UWEKAJI MUKTADHA KATIKA MIRADI YA KUKABILIANA NA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Mbinu za sasa za miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia zinatofautiana katika maeneo mbalimbali, zikiathiriwa na muktadha wa eneo, kaida za kitamaduni na rasilimali zinazopatikana. Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yapo katika mstari wa mbele wa kuweka muktadha katika viwango vya kimataifa vya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia ili viendane na mazingira haya ya kipekee, mara nyingi yakikabiliana na hali changamano za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika miktadha yote iliyotathminiwa, ushirikishaji wa jamii ya eneo umekuwa kiini cha kuhakikishwa kwamba miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia inakubaliwa na inawafaa watu ambao inahudumia. Mashirika ya kutetea haki za wanawake na mashirika yanayoongozwa na wanawake yaliripoti kwamba utohozi wa huduma ili kutimiza mahitaji ya vikundi vilivyotengwa, kama vile watu wa Asili nchini Guatemala na wakimbizi nchini Yordani, ungali na kipaumbele kikuu. Mwisho, kukuza uwezo wa mashirika ya eneo kungali suala linalozingatiwa sana, hasa katika muktadha wa ufadhili mchache na changamoto za uendeshaji.

Nchini DRC, mashirika yanayoongozwa na wanawake yamejumuisha utoaji wa misaada ya riziki na huduma zinazoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia, huku ikiwapatia wateja fursa za kupata ujuzi mpya kama vile utengenezaji wa sabuni na utengenezaji wa makaa. Mbinu hii haishughulikii hatari za kiuchumi tu, bali pia inawawezesha wateja kuwa na uhuru wa kifedha na hivyo kupunguza utegemeaji wao wa mbinu zenye madhara za kukabiliana na hali yao, kama vile ngono ya kujikimu. Kujumuishwa kwa riziki na huduma zinazoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia pia husaidia kuimarisha uthabiti wa jamii. Hata hivyo, changamoto za usalama na upungufu wa ufadhili unaendelea kuweka vizuizi kwa upanuzi wa miradi hii katika maeneo mengine yaliyoathiriwa na mizozo na ya mbali.

Nchini Guatemala, mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yaliwekea muktadha miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia ili kutimiza mahitaji ya jamii za Asili, hasa katika maeneo ya mashambani. Mashirika ya eneo yanayoongozwa na wanawake hufanya kazi na viongozi wa jamii ili kuhakikisha kwamba miradi imeeleweka na kukubaliwa, mara nyingi wakitafsiri nyenzo katika lugha za kiasili kaa vile Mam na K'iche'. Pia wanatumia vielelezo vya kuonekana na simulizi ili kushirikisha vikundi vyenye uwezo wa chini wa kusoma na kuandika. Hata hivyo, bado kuna kizuizi kikubwa cha kupata ufadhili wa kutosha wa kupanua juhudi hizi katika maeneo ya mbali. Utohozi huu unazingatia kuboresha ufikiaji na kuhakikisha kwamba wateja wanajihisi huru kutafuta usaidizi.

Nchini Yordani, utohozi wa huduma zinazoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia umekabiliana na kaida za kijamii nchini humo zinazowakatisha wanawake tamaa ili wasipate usaidizi, hasa katika maeneo yaliyoshikilia ukale zaidi. Vituo tamba vya kutoa huduma zinaoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia ni mfano mmoja wa suluhisho la ubunifu la tatizo hili, huku vikitoa huduma kwa faragha na kwa njia inayozingatia utamaduni. Maeneo salama katika jamii pia yanatoa mbadala wa makao ya hifadhi ya umma, ambapo unyanyapaa unaweza kuwa kizuizi kikubwa. Hata hivyo, uhaba wa ufadhili endelevu unazuia uwezo wa kupanua mbinu hizi nchini kote. Kuwashirikisha wanaume na wavulana katika kubadilisha kaida za jinsia ni muhimu sana katika kushughulikia ukosefu wa usawa wa kijinsia na katika kuzuia unyanyasaji katika siku zijazo.

# MBINU ZINAZOTUMIWA NA MASHIRIKA YANAYOONGOZWA NA WANAWAKE NA MASHIRIKA YA KUTETEA HAKI ZA WANAWAKE KATIKA KUWEKEA MUKTADHA MIRADI YA KUKABILIANA NA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yanaripoti kuwa yanatumia mbinu kadhaa kuwekea muktadha na kutekeleza miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Yote yanaziba pengo kati ya viwango vya kimataifa na hali halisi katika eneo, yakihakikishwa kwamba miradi ina ufanifu, ni endelevu na inazingatia waathiriwa. Kuelewa mbinu hizi kunatoa maarifa muhimu ya jinsi mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yantimiza mahitaji ya eneo huku yakitetea mabadiliko ya kimfumo. Mbinu hizi haziimarishi ufaafu wa miradi tu, bali pia zinaimarisha umiliki na uwajibikaji wa kieneo.

**MBINU ZA NDANI YA JAMII**

Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake huwekea kipaumbele kushirikisha jamii za eneo ili kuhakikishwa kwamba miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia imerekebishwa kulingana na mahitaji na hali mahususi za watu yanaohudumia. Kwa kushirikiana na viongozi wa eneo, mashirika ya eneo na waathiriwa, huwa yanahakikisha kwamba miradi inafaa utamaduni na kukubaliwa na wengi.

**KUKUZA UWEZA KWA AJILI YA UMILIKI WA ENEO**

Ni muhimu sana kujenga uwezo wa wahusika wa eneo ili kuhakikisha uendelevu na uongozi wa eneo. Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake hutoa mafunzo na rasilimali kwa mashirika ya eneo, yakiyawezesha kusimamia miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kivyao na kupunguza utegemeaji wa ufadhili kutoka nje.

**MBINU ZINAZOZINGATIA WAATHIRIWA**

Miradi iliyoundwa na mahitaji na mapendeleo mahususi ya waathiriwa kama kiini huhakikisha juhudi zenye ufanifu zaidi. Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake husikiliza waathiriwa na kujumuisha maoni yao katia uundaji wa miradi, yakitoa usaidizi mahususi wa kisaikolojia, usaidizi wa kisheria na uwezeshaji wa kiuchumi.

**TEKNOLOJIA NA UBUNIFU KATIKA UTOAJI WA HUDUMA**

Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yanatumia teknolojia kufikia jamii ambazo ni ngumu kufikia na kupanua mbinu zao za utoaji huduma. Majukwaa tamba, huduma za afya kupitia simu na mawasiliano dijitali yamekuwa muhimu sana katika kuhakikisha kwamba wateja wanaweza kupata huduma, hasa katika maeno yenye miundomsingi duni.

**UTETEZI WA MABADILIKO YA SERA NA SHERIA**

Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake hufanya utetezi ili kuelekeza sera za eneo na za kitaifa kuhusiana na unyanyasaji wa kijinsia, na hivi kuhakikisha kwamba mifumo ya kisheria si jumuifu tu, bali pia inatekelezwa ipasavyo. Yanashirikiana na serikali na mashirika ya kimataifa kutetea ulinzi wa wateja na kufunguliwa mashtaka kwa wahalifu.

Kwa mfano, nchini Yordani, mashirika ya kutetea haki za wanawake yanatetea sheria kali zaidi dhidi ya unyanyasaji wa kingono na unyanyasaji wa kijinsia, yakipigania mabadiliko ya sera ili kulinda na kusaidia waathiriwa vyema zaidi.

**USHIRIKIANO NA UKUZAJI WA MAHUSIANO**

Ushirikiano kati ya mashirika ya eneo na ya kimataifa ni muhimu sana kwa ajili ya kushiriki rasilimali, maarifa na ujuzi. Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake hukuza ushirika unaoimarisha upana na ufanifu wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia.

# MIELEKEO KATIKA UWEKAJI MUKTADHA KATIKA MIRADI YA KUKABILIANA NA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Mbinu za kuweka muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia zinatofautiana kwa wadau tofauti, zikidhihirisha vipaumbele vyao vya kipekee, wajibu wa uendeshaji na rasilimali walizo nazo.

### WAFADHILI KWA SASA WANAZINGATIA MATOKEO YANAYOWEZA KUPIMWA

Wafadhili wanaripoti kwamba wanaweka kipaumbele kufadhili mapendekezo yanayodhihirisha matokeo dhahiri yanayoweza kupimwa na yanayopatana na vipaumbele vya kimataifa. Hata hivyo, mara nyingi hawana mbinu rasmi za kutathmini kiwango ambacho mapendekezo yanajumuisha uwekaji muktadha zaidi ya upatano wa jumla na viwango vya kimataifa.

Kwa mfano, mfadhili mmoja alitaja umuhimu wa kushughulikia hali halisi katika eneo, kama vile mwingiliano wa jinsia, katika mapendekezo ya miradi lakini alikiri kwamba mifumo ya tathmini ya shirika lake kimsingi inazingatia matokeo yanayoweza kupimwa, kama vile idadi ya wateja waliofikiwa, badala ya kutathmini ubora wa utohozi kulingana na muktadha.

Hali hii inazidishwa na ukweli kwamba wafadhili, ijapokuwa wanatambua umuhimu wa kurekebisha miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kulingana na hali halisi katika eneo, wanaripoti vikwazo vya ufadhili mara nyingi huzuia uwezo wa mashirika kuweka muktadha kikamilifu. Baadhi ya wafadhili walitaja changamoto ya kuweka uwiano mzuri kati ya kuweka mbinu madhubuti za uwajibikaji na kutoa uhuru unaohitajika kufanya utohozi katika eneo.

### MASHIRIKA YA KIMATAIFA YASIYO YA SERIKALI HUFANYA MAREKEBISHO MADOGO LAKINI HUWEKA MUKTADHA KIKAMILIFU KWA NADRA

Mara nyingi mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali huwa wahusika wa kati, yakitekeleza miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kwa niaba ya wafadhili na kushirikiana na washirika wa eneo. Juhudi zao za kuweka muktadha zinadhihirisha faida na vikwazo vya kufanya kazi katika miktadha tofauti.

Mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali hutumia mifumo iliyosawazishwa ili kuhakikisha ulinganifu katika maeneo mbalimbali. Mifumo hii mara nyingi hurekebishwa katika safu ya vitendo wala si kufanywa upya kuendana na muktadha wa eneo. Hali hii huhakikisha upatano na vipaumbele vya wafadhili lakini inaweza kupunguza kiwango cha uwekaji muktadha.

Kwa mfano, nchini Yordani, baadhi ya mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali yamerekebisha utoaji wa huduma zao kujumuisha vituo tamba, hali inayowezesha upatikanaji wa huduma kwa faragha katika maeneo yanayoshikilia ukale. Hata hiyo, miundo iliyojengewa mradi mara nyingi haibadiliki katika maeneo mbalimbali, hali ambayo hudunisha uelekevu wa miradi kwa changamoto mahususi za eneo.

Licha ya juhusi za kushirikisha washiriki wa eneo, mashirika mengi ya kimataifa yasiyo ya serikali yanaripoti changamoto katika kujumuisha maoni ya maeneo kikamilifu kwa sababu ya vipindi vifupi vya ufadhili na vipaumbele vilivyowekwa na wafadhili. Nchini Guatemala, mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali yanaripoti kwamba ukosefu wa uhuru katika ufadhili ulizuia uwezo wao wa kutohoa miradi kulingana na mahitaji ya wanawake wa Asili kwa ufanifu. Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yamejikita katika jamii wanazohudumia, hali inayowawezesha kuweka muktadha kwa ufanifu katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Hata hivyo, yanaripoti kwamba juhudi zao mara nyingi huzuiwa na upungufu wa rasilimali na ukosefu wa uwezo wa kufanya maamuzi katika ushirikiano na mashirika makubwa zaidi.

## MASHIRIKA YANAYOONGOZWA NA WANAWAKE NA MASHIRIKA YA KUTETEA HAKI ZA WANAWAKE HUSHIRIKIANA NA JAMII LAKINI HUKABILIWA NA VIZUIZI VYA UFADHILI.

Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake husisitiza ushirikishaji wa jamii kama kipengele muhimu cha uwekaji muktadha. Hii ni pamoja na ujumuishaji wa wateja na viongozi wa jamii katika uundaji wa miradi na matumizi ya nyenzo zinazoendana na utamaduni katika utoaji wa huduma. Kwa mfano, nchini Guatemala, mashirika yanayoongozwa na wanawake yalibuni njia za kusimulia hadithi kwa kutumia vielelezo ili kuwashirikisha wanawake wa Asili wenye viwango vya chini vya kusoma na kuandika, na hivyo kuimarisha ufikiaji na ufaafu wa nyenzo za mradi.

Licha ya ujuzi wao wa eneo, mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yangali yanategemea sana ufadhili wa nje, ambao mara nyingi ni wa muda mfupi na wenye mipaka. Hali hii hudunisha uwezo wa mashirika haya kuweka muktadha katika miradi au kupanua mbinu fanifu. Kwa mfano, nchini DRC, baadhi ya mashirika yanayoongozwa na wanawake yanaripoti ugumu wa kupata ufadhili wa kupanua miradi yenye mafanikio inayojumuisha misaada ya riziki ambayo inakabiliana na matishio ya kiuchumi ya waathiriwa.

Zaidi na ziadi, mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yanatetea huduma zinazozingatia dhiki na miradi inayozingatia waathiriwa, yote ambayo huzingatia kutimiza mahitaji ya sasa ya waathiriwa na wakati huo huo kuheshimu uhuru wao wa kufanya maamuzi. Kwa mfano, nchini Yordani, mashirika yanayoongozwa na wanawake yamesisitiza umuhimu wa usaidizi mahususi wa kisaikolojia, ili kuhakikisha kwamba wateja wanapokea huduma inayoendana na mahitaji yao hasa na inayotambua masuala ya kitamaduni.


Picha imepigwa na **Billy Mutai kwa ajili ya IRC**



*Picha imepigwa na* ***Martha Tadesse***

## KUTATHIMINI UFANIFU WA UWEKAJI MUKTADHA KATIKA MIRADI YA KUKABILIANA NA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Kutathmini ufanifu wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia iliyowekewa muktadha ni muhimu sana katika kuelewa ikiwa inatimiza mahitaji ya wateja na kukabiliana na changamoto za miktadha mahususi. Ni muhimu sana kutathmini matokeo ya miradi na pia ufaafu na ufanifu wa miradi hiyo katika kutoa usaidizi unaoweza kufikiwa na unaofaa kwa wateja katika miktadha mbalimbali. Mchakato huu wa kutathmini mara nyingi hutegemea maoni ya jamii, tathmini za kabla na baada na viashiria vya tabia, ijapokuwa kuna changamoto kubwa katika kupima mafanikio ya muda mrefu na kutambua sehemu zinazoweza kuendelea kuboreshwa.

Hata hivyo, ufanifu hutathminiwa kwa njia tofauti na wadau tofauti.

Kwa mfano, wafadhili mara nyingi husisitiza matokeo yanayoweza kupimwa, kama vile idadi ya waathiriwa waliohudumiwa au upatikanaji wa huduma, ili kukadiria athari ya ufadhili wao. Hata hivyo, kutegemea vipimo vya idadi kunaweza kudunisha uelewa wa athari za kina zaidi za juhudi za kuweka muktadha. Baadhi ya wafadhili wameeleza hamu ya kupata data ya maelezo, ikiwa ni pamoja na maarifa ya mabadiliko katika mitazamo ya jamii, uwezeshaji wa waathiriwa na mabadiliko katika kaida za kijinsia. Licha ya hayo, mbinu za kupata maoni kama vile majadiliano ya vikundi na tafiti za jamii hazitumika sana kutathmini athari zisizohesabika za miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia.

Mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali yalitaja kwamba yanatumia zana kama vile uchambuzi wa kinga, majadiliano ya vikundi na usaili ili kutathmini miradi iliyowekewa muktadha. Hata hivyo, yalitaja pia kwamba tathmini zao mara nyingi pia hudunishwa na vipindi vifupi vya ufadhili, ambavyo havitoi nafasi nzuri ya tathmini za athari za muda mrefu. Kwa mfano, nchini Guatemala, mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali yalieleza changamoto za kufuatilia ufanifu wa muda mrefu wa nyenzo zilizotoholewa kulingana na utamaduni kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali hususan za ufuatiliaji na tathmini.

Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yaliripoti kuwa yanazingatia sana tathmini zinazoendeshwa na jamii, ambapo maoni ya waathiriwa yana nafasi muhimu katika kukadiria ufanifu wa miradi. Nchini DRC, mashirika yanayoongozwa na wanawake yalitumia maoni ya waathiriwa kurekebisha miradi ya kutoa misaada ya riziki na kuhakikisha kwamba inatimiza mahitaji ya kiuchumi ya waathiriwa. Hata hivyo, yalitaja changamoto katika kupanua mbinu hizi za tathmini kwa sababu ya upungufu wa rasilimali za kifedha zinazohitajika kwa ukusanyaji endelevu wa data.



### MIRADI JUMUISHI ILIFANYA KAZI VYEMA NCHINI DRC

Nchini DRC, kujumuisha usaidizi wa riziki katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kulitimiza mahitaji ya kiuchumi na pia ya kisaikolojia ya waathiriwa. Mashirika yanayoongozwa na wanawake yameripoti mafanikio katika kuwasaidia waathiriwa kupata uhuru wa kifedha, ingawa changamoto za upanuzi na uendelevu wa muda mrefu zingalipo kwa sababu ya vikwazo vya kifedha na matishio ya usalama. Wafadhili walitambua mafanikio ya mbinu hii inayowasaidia wateja kupata uhuru wao tena na kupunguza utegemeaji wa mbinu zenye madhara za kukabiliana na hali yao, kama vile ngono ya kujikimu. Hata hivyo, walitaja haja ya tathmini madhubuti zaidi ili kuonyesha matokeo ya muda mrefu.

### NYENZO ZILIZOREKEBISHWA KULINGANA NA MUKTADHA ZILIKUZA UFIKIAJI WA HUDUMA NCHINI GUATEMALA

Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali yalibuni vielelezo vya kuonekana na kutafsiri maudhui ya mradi kwa lugha za asili ili kuhakikisha kwamba watu wenye uwezo mdogo wa kusoma na kuandika wanaweza kufikia huduma za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Hatua hii imeimarisha sana ufahamu na matumizi ya huduma katika jamii za Asili. Hata hivyo, mashirika yanayoongozwa na wanawake yaliangazia haja ya kuendelea kwa ufadhili ili yapanue nyenzo hizi zinazozingatia utamaduni kutoka awamu ya majaribio.

### HUDUMA TAMBA ZILIWASAIDIA WANAWAKE MASHAMBANI HUKO YORDANI

Huduma tamba zimekuwa za msaada katika kuwafikia wanawake mashambani, ambako kuna unyanyapaa wa kutumia makazi ya hifadhi ya kawaida. Huduma hizi hutoa usaidizi wa kisheria, msaada wa kisaikolojia na kijamii na utunzaji wa afya, ili kuhakikisha kwamba wateja wanaweza kupata huduma kwa faragha. Hata hivyo, mashirika yanayoongozwa na wanawake na wafadhili walieleza shaka kuhusu gharama ya kupeleka huduma hizi nchini kote.

# 2

## SEHEMU YA 2

# Ufadhili na ugawaji wa rasilimali

Ufadhili wa kutosha na usawa katika ugawaji wa rasilimali ni muhimu sana kwa mafanikio ya miradi iliyowekewa muktadha ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Ufadhili wa kuweka muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kwa kawaida umefanywa na wafadhili wa kimataifa, wakizingatia kuhakikisha uwajibikaji na kupata matokeo yanayoweza kupimwa. Hata hivyo, kiwango ambacho ufadhili unashughulikia uwekaji muktadha bado ni tatizo muhimu.

Wafadhili walidhihirisha mwelekeo wao wa kusisitiza kufadhili miradi inayopatana na vipaumbele na matokeo yanayoweza kupimwa. Ijapokuwa wafadhili wanatambua umuhimu wa kutimiza mahitaji ya eneo, njia za ufadhili mara nyingi husisitiza kufanya kazi kupitia washirika thabiti wa kimataifa au kitaifa, huku ufadhili wa moja kwa moja kwa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake ukiwa mdogo sana. Changamoto za uwajibikaji na kujenga uwezo zilitajwa kama vizuizi vya kuongeza ufadhili wa moja kwa moja kwa mashirika ya eneo. Mmoja wa watoa taarifa wakuu alieleza shaka kuhusu uwezo wa kusimamia fedha wa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake. Pia alitaja hali ambapo mashirika ya eneo hayakuwa na uaminifu katika kutoa taarifa zao za kifedha.

Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake yaliangazia upungufu wa ufadhili wa moja kwa moja kwa mashirika ya eneo, hasa yale yanayoongozwa na wanawake. Nchini Guatemala, mashirika yanayoongozwa na wanawake yalieleza kwamba utegemeaji wao wa wahusika wa kati wa kimataifa hudunisha uwezo wao wa kupata rasilimali za kifedha za kutosha kwa ajili ya miradi iliyowekewa muktadha. Nchini DRC, mashirika yanayoongozwa na wanawake yaliripoti kwamba wafadhili mara nyingi huweka mipaka ya jinsi fedha zinaweza kutumiwa na hivyo kudunisha uwezo wao wa kutohoa miradi kulingana na hali halisi ya eneo.

## VIKWAZO VYA UFADHILI HUZUIA UWEKAJI MUKTADHA KATIKA MIRADI YA KUKABILIANA NA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Licha ya umuhimu unaojulikana na kauli za kuweka kipaumbele kwa uwekaji muktadha kwa ajili ya ufanisi wa miradi, wadau walitambua vikwazo kadhaa vya kupata na kugawa rasilimali kwa ufanifu. Vikwazo hivi, ambavyo vinafahamika vyema katika sekta ya uhisani, huathiri upatikanaji wa rasilimali za kuweka muktadha katika miradi. Vikwazo hivi ni pamoja na:

**MBINU ZA UFADHILI HAZIPINDIKI**

Hali ya kutobadilika kwa ufadhili ni tatizo linalojitokeza mara kwa mara. Kwa mfano, mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake nchini Yordani na DRC yalieleza kwamba matakwa ya wafadhili mara nyingi huzingatia matokeo yaliyosawazishwa, hali isiyotoa nafasi ya kutosha ya kutohoa miradi kulingana na maoni ya mudahalisi kutoka kwa jamii.

**VIPINDI VYA UFADHILI NI VIFUPI MNO**

Ufadhili wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia mara nyingi hutolewa kwa muda mfupi, hali inayoifanya vigumu kupanga na kutekeleza miradi endelevu ya muda mrefu iliyowekewa muktadha. Mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake nchini DRC yanataja kwamba shinikizo la kutimiza malengo ya muda mfupi mara nyingi huvuta fikra mbali na kukabiliana na sababu hasa za unyanyasaji wa kijinsia kupitia miradi mahususi.

**MASHIRIKA YA ENEO HUPOKEA UFADHILI USIOTOSHA WA SHUGHULI ZA MSINGI**

Ni nadra kwa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake kupokea ufadhili wa shughuli za msingi; ufadhili huo ni muhimu sana katika kujenga uwezo wa shirika na kuhakikisha uendelevu wa miradi iliyowekewa muktadha. Nchini Guatemala, mashirika ya eneo yaliripoti kwamba ukosefu wa ufadhili wa shughuli za msingi unadunisha uwezo wao wa kushiriki katika utetezi au kupanua huduma zao.


*Picha imepigwa na Adrienne Surprenant*

3

## SEHEMU YA 3

# Vizuizi vya uwekaji muktadha

Licha ya hitaji bayana la uwekaji muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, vizuizi kadhaa vinadunisha utekelezaji wa mchakato huu kwa ufanifu. Vizuizi hivi vinatokana na kaida za kitamaduni, mipaka ya ufadhili, vikwazo vya ugavi na haja ya uratibu bora zaidi kati ya wahusika wa eneo na wa kimataifa. Kwa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake, vizuizi vya uwekaji muktadha mara nyingi huzidishwa na upungufu wa rasilimali, mifumo isiyobadilika ya wafadhili, mahitaji yanayobadilika ya waathiriwa, hasa katika mazingira changamano ya kibinadamu au ya mizozo. Sehemu hii inachunguza vizuizi hivi na jinsi vinavyoathiri juhudi za mashirika yanayoongozwa na wanawake, mashirika ya kutetea haki za wanawake, mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali na za wafadhili za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kwa ufanifu na kulingana na muktadha.

### VIZUIZI VYA UTAMADUNI NA VYA KIJAMII

Vizuizi mbalimbali vya utamaduni na vya kijamii huathiri uwezo wa kufikia huduma na kukubaliwa kwa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Vizuizi hivi vinaweza kukwamisha sana ufanifu wa miradi iliyowekewa muktadha ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia.

Kwa mfano nchini Yordani, mashirika yanayoongozwa na wanawake yaliripoti kwamba kaida za kitamaduni zinazoshikilia ukale mara nyingi huwazuia wanawake kutumia makazi ya kawaida ya hifadhi. Unyanyapaa wa jamii kwa wateja wanaotafuta usaidizi unafanya hali hii iwe mbaya zaidi. Ili kukabiliana na hali hii, mashirika yanayoongozwa na wanawake yalianza kutumia vituo tamba vinavyotoa huduma kwa faragha katika jamii, lakini changamoto ingalipo ya kufikia vikundi vya watu waliotengwa zaidi ambao huenda wasiweze kufikia huduma tamba.

Nchini Guatemala, wanawake wa Asili wanakumbwa na vizuizi vya kipekee vya utamaduni vinavyowazuia kupata huduma za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, hasa katika maeneo ya mbali. Ijapokuwa mashirika yanayoongozwa na wanawake yametohoa miradi ili izingatie utamaduni na kutumia vielelezo vya kuonekana, mitazamo iliyokita mizizi ya mfumo dume katika baadhi ya jamii inaendelea kuzuia wanawake kushiriki katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia.



Picha imepigwa na **Jacob Zocherman** kwa ajili ya IRC

## VIZUIZI VYA UFADHILI NA RASILIMALI

Upungufu wa ufadhili na rasilimali unaendelea kuwa kizuizi kikubwa kwa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake, hasa katika kuweka muktadha ili miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia itimize mahitaji ya eneo. Ijapokuwa wafadhili husisitiza umuhimu wa uwajibikaji na matokeo yanayoweza kupimwa, ukosefu wa ufadhili wenye uhuru na wa muda mrefu mara nyingi huzuia juhudi za uwekaji muktadha zisifike upeoni.

Wafadhili wanakiri kuwa kuna ukosefu wa ufadhili wa moja kwa moja kwa mashirika ya eneo yanayoongozwa na wanawake na ya kutetea haki za wanawake. Badala yake, ufadhili hupitia mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali au mashirika ya kitaifa, hali inayodunisha uwezo wa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake wa kudhibiti ufadhili moja kwa moja na kuweka muktadha katika miradi kwa njia inayoendana na mahitaji ya eneo.

Nchini DRC, mashirika yanayoongozwa na wanawake yaliafiki kwamba mara nyingi hawana ufadhili wa moja kwa moja, hali ambayo huongeza muda unaotumika ili fedha zifikie wahusika wa eneo, na pia kuweka kizuizi katika uhuru wa kufanya maamuzi katika eneo. Nchini Guatemala, mashirika yanayoongozwa na wanawake yaliripoti kwamba ufadhili unaotegemea miradi mara nyingi hudunisha uwezo wao wa kujenga miradi endelevu ya muda mrefu inayolingana na mahitaji hasa ya waathiriwa.

Wateja wenyewe pia walitaja kwamba ukosefu wa rasilimali mara nyingi hudunisha manufaa yanayodhaniwa kutokana na kushiriki. Kama mshiriki mmoja alivyoeleza,

> ***"Manufaa hupungua, na tunaporudi nyumbani, tunarudi mkono mtupu."***

Hii inaangazia haja ya kuongeza ugawaji wa rasilimali ili kuhakikisha kwamba washiriki wanahisi manufaa halisi na ya kudumu ya miradi hiyo.

## VIZUIZI VYA UGAVI NA UENDESHAJI

Utekelezaji wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia iliyowekewa muktadha unahitaji utohozi kulingana na vizuizi mahususi vya ugavi ka uendeshaji katika kila eneo. Katika maeneo yenye mizozo, ya mbali na yenye miundomsingi duni, vizuizi vya ugavi huwa vikubwa zaidi.

Kwa mfano, nchini DRC, hali ya usalama na kufurushwa kwa jamii kunaleta vizuizi vikubwa kwa utoaji wa huduma. Mashirika yanayoongozwa na wanawake yalitaja kwamba ingawa yametohoa huduma zao kutimiza mahitaji ya waathiriwa, matatizo kama vile ukosefu wa usafiri na miundomsingi duni huzuia ufikiaji wa maeneo salama na miradi ya kutoa misaada ya riziki. Licha ya hayo, mashirika yanayoongozwa na wanawake yanaendelea kutoa huduma lakini yanaripoti kwamba uwezo wao wa kuzipanua mara nyingi huzuiwa na ukosefu wa rasilimali.

Nchini Yordani, licha ya utohozi wa huduma tamba, umbali wa kijiografia na ugumu wa kufikia baadhi ya maeneo ya mashambani unaendelea kuzuia ufikiaji wa huduma hizi. Mashirika yanayoongozwa na wanawake yanakabiliwa na changamoto katika kushirikiana na serikali za mitaa ili kuhakikisha maeneo salama yanaanzishwa katika maeneo ya mbali ambapo wanawake wahamiaji wanaweza kuwa katika hatari kubwa zaidi.

## VIZUIZI VYA MASHIRIKA NA URATIBU

Uwekaji muktadha kwa ufanifu unahitaji ushirikiano na uratibu kati ya wahusika wa eneo, mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali, mashirika yanayoongozwa na wanawake, mashirika ya kutetea haki za wanawake na wafadhili. Maarifa kutoka kwa mahojiano na majadiliano ya vikundi yaliangazia kwamba changamoto za mashirika na za uratibu mara nyingi huzuia utekelezaji fanifu wa miradi. Kwa mfano, watoa habari wakuu kutoka mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake walitaja kwamba kutojumuishwa vile katika michakato ya kufanya maamuzi na ukosefu wa mawasiliano ya moja kwa moja na wafadhili mara nyingi hudunisha uwezo wao wa kurekebisha miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kulingana na mahitaji ya eneo. Vivyo hivyo, washiriki katika majadiliano ya vikundi walieleza shauku yao kuhusu utoaji huduma uliogawanyika. Walisisitiza kwamba ushirikiano bora kati ya wadau unaweza kuimarisha ufikiaji na ufanifu wa miradi.

Mashirika mengi ya kimataifa yasiyo ya serikali yalitaja kwamba uratibu kati ya wahusika wa eneo na wa kimataifa mara nyingi hudunishwa na mipaka ya mashirika. Kwa mfano, nchini Guatemala, mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali na mashirika yanayoongozwa na wanawake yalitaja ugumu uliopo katika kupatanisha malengo yao kwa sababu ya vipaumbele vyao tofauti au upungufu wa ufadhili. Ukosefu huu wa upatano unaweza kuchelewesha juhudi za kuweka muktadha na kusababisha kugawanyika kwa juhudi za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia.

Mashirika yanayoongozwa na wanawake nchini Yordani yaliripoti tatizo sawa na hilo, ambapo uratibu kati ya washirika wa eneo na wa kimataifa wakati mwingine huwa mgumu, hasa katika kushiriki mbinu bora na rasilimali. Washirika wa eneo mara nyingi walihisi kutengwa katika michakato ya kufanya maamuzi, hali iliyoathiri uwezo wao wa kutoa suluhu mahususi kwa muktadha.

Wafadhili walisisitiza nafasi muhimu ya uratibu bora na washirika wa eneo katika kuimarisha upatano wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na vipaumbele vya eneo. Waliangazia umuhimu wa kuhusisha wahusika wa eneo katika kuratibu vikundi vya mashirika ili kuhakikisha kwamba miradi inaambatana na muktadha na inazingatia waathiriwa. Vilevile, wafadhili walitoa wito wa kuimarisha ushirikiano kati yao wenyewe, na mashirika ya eneo na washirika wa utekelezaji ili kuleta ufanisi katika juhudi na kuepuka urudiaji. Wafadhili wanaamini kwamba kwa kuboresha mbinu za kushiriki maarifa na kukuza ushirikiano, miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia inaweza kujumuisha mafunzo yaliyopatikana na mbinu bora, na hivyo kuifanya yenye ufanisi na matokeo bora zaidi.


*Picha imepigwa na **Ojong Spencer***

4

## SEHEMU YA 4
# Hitimisho

Uwekaji muktadha ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia ni fanifu, faafu na endelevu katika kushughulikia mahitaji mahususi ya wateja katika mazingira mbalimbali. Ijapokuwa viwango vya kimataifa vya kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia vinatoa mwongozo muhimu, utekelezaji bora wa mifumo hii unahitaji utohozi wa maana ili kuendana na hali halisi ya eneo ya kitamaduni, kijamii na kisheria. Mashirika ya eneo, hasa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake, yana wajibu muhimu katika mchakato wa uwekaji muktadha, lakini yanakabiliwa na vizuizi vikubwa vya ufadhili, uwezo na uratibu. Zaidi na zaidi, wafadhili wanatambua umuhimu wa uwekaji muktadha, lakini mbinu zilizopo za ufadhili hazibadiliki kwa urahisi, mara nyingi zikiweka kipaumbele kwa matokeo ya muda mfupi kuliko unyumbufu wa muda mrefu unaohitajika katika utohozi wa kufaa muktadha.

Maarifa haya yana athari muhimu kwa utendaji na kwa sera:

**KWA WATAALAMU,** uwekaji muktadha sharti ujumuishwe katika upangaji, utekelezaji na tathmini za miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Wahusika wa eneo, ikiwa ni pamoja na mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake, wanafaa kupewa udhibiti zaidi wa uundaji wa miradi na ugawaji wa rasilimali, kupitia ufadhili wenye uhuru unaowawezesha kuitikia mahitaji yanayoibuka.

**KWA WATUNGA SERA,** serikali na mashirika ya kimataifa yanafaa kuwekea kipaumbele ufadhili wa muda mrefu na wenye uhuru kwa mashirika ya eneo, huku yakizingatia kukuza uwezo ili kuhakikisha wahusika wa eneo wanaweza kuendesha miradi iliyowekewa muktadha. Vilevile, sera mpya zinafaa kutambua haja ya unyumbufu katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, ili kuhakikisha kwamba viwango vya kimataifa vinaweza kutekelezwa kwa ufanifu katika miktadha mbalimbali ya kitamaduni na kisheria.

**KATIKA UTENDAJI,** wafadhili, mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali na mashirika ya eneo yanafaa kuimarisha mbinu za kupata maoni ambazo zinaitika mahitaji ya wateja. Wafadhili na watekelezaji wanastahili kushirikiana kwa karibu na wadau wa eneo ili kuhakikisha ufaafu kwa muktadha na uzingatiaji wa masuala ya kitamaduni.



*Picha imepigwa na* ***Martha Tadesse kwa ajili ya IRC***

# KIAMBATISHO CHA 1
# Mbinu

Utafiti ulifanywa katika nchi tatu—Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Guatemala na Yordani—ili kuonyesha tofauti katika maeneo na kuchunguza juhudi za uwekaji muktadha katika hali tofauti za kijiografia, kijamii na kibinadamu.

Tumetumia mbinu mseto kwa kujumuisha data ya msingi na ya upili iliyopatikana kutoka uchambuzi wa machapisho, mahojiano na watoa taarifa wakuu na majadiliano ya vikundi. Hii imewezesha tathmini madhubuti ya mielekeo, changamoto na fursa katika kuwekea muktadha miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia.

Mbinu hii inahakikisha kwamba maarifa na mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yanategemea ushahidi, ni ya kina na yanawakilisha mitazamo ya wadau anuai. Mbinu hii ya safu mbalimbali inaangazia umuhimu wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia iliyowekewa muktadha huku ikishughulikia vizuizi vya kimfumo na fursa za kuimarisha.

### UCHAMBUZI WA MACHAPISHO

Uchambuzi wa machapisho ulipitia maandiko, ripoti na data ya upili iliyopo kutoka mashirika muhimu, ikiwa ni pamoja na UN Women, WHO, Human Rights Watch, ReliefWeb, UNHCR, UNICEF na IRC. Uchambuzi huo ulitambua mbinu bora na kanuni za kuweka muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Inajumuisha uchambuzi wa miongozo na mifumo ya kimataifa kama vile *Nyenzo ya Kuweka Muktadha katika Viwango vya Chini vya Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia, Mwongoza wa IASC wa Juhudi za Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia* na sera kutoka UNHCR na UNICEF, ambazo zinasisitiza umuhimu wa kuweka muktadha katika miradi ili kulingana na mahitaji mahusus ya jamii za eneo.

Uchambuzi huo wa machapisho ulitambua mada muhimu katika miradi yenye ufanifu ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, kama vile uwekaji muktadha, umiliki wa eneo, mbinu zinazozingatia waathiriwa, ushirikiano wa wadau mbalimbali na haja ya ufadhili wenye uhuru na wa muda mrefu. Uchambuzi huu uligundua kwamba miradi sharti ilenge miktadha mahususi, ikizingatia masuala kama desturi za kitamaduni, kaida za kijinsia na mahitaji ya kipekee ya vikundi mbalimbali vya watu, kama vile watu waliofurushwa na pia wanawake na wasichana walio katika hatari.

### MAHOJIANO NA WATOA TAARIFA WAKUU

Mahojiano yaliyoweka mpangilio kwa kiasi fulani yalifanywa na watoa taarifa wakuu 20, wakiwemo wafadhili na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali, mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake katika nchi tatu. Mahojiano haya yalichunguza:

- Vipaumbele vya wafadhili na changamoto wanazokumbana nazo katika kufadhili miradi iliyowekewa muktadha ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia
- Wajibu wa mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali katika kuweka muktadha katika mifumo ya kimataifa ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na kusaidia mashirika ya eneo
- Uzoefu wa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake katika kuweka muktadha katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, ukizingatia ufadhili wa kifedha na wa kiufundi.

Mahojiano hayo yalitoa maarifa ya jinsi mwingiliano wa mashirika, kama vile changamoto zinazokumba mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake katika kupata ufadhili wa kutosha na vizuizi vya kuweka muktadha kikamilifu katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Yaliibua pia viwango tofauti vya usaidizi unaotolewa kwa mashirika yanayoongozwa na wanawake na mashirika ya kutetea haki za wanawake katika kuweka muktadha wao mahususi katika viwango vya kimataifa.



Picha imepigwa na **Maheder Haileselassie**

## MAJADILIANO YA VIKUNDI

Jumla ya majadiliano 28 ya vikundi yalifanywa na wateja wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, yakijumuisha vikundi mbalimbali vya watu nchini DRC, Guatemala na Yordani. Kila majadiliano yalijumuisha takriban washiriki 10 kutoka jamii za wenyeji na katika miktadha ya watu waliofurushwa mwakao. Lengo la majadiliano lilikuwa:

- Kutathmini ufaafu na ufanifu wa miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kwa mtazamo wa mwathiriwa
- Kutambua vizuizi vya kufikia huduma na mapendekezo ya kuimarisha hali
- Kuelewa jinsi nyenzo na huduma zilizotoholewa vyema kulingana na utamaduni zilikabiliana na changamoto za eneo.

Mahojiano ya vikundi yaliangazia umuhimu wa kurekebisha miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia kulingana na mahitaji mahususi ya wateja, huku washriki wakitaja athari za vizuizi kama vile unyanyapaa, uwezo duni wa kupata rasilimali na nyenzo ambazo hazijajainibishwa ipasavyo.

## UTEUZI WA SAMPULI NA UKUSANYAJI WA DATA

Mkakati wa kuteua sampuli ya utafiti huu ulihakikisha uwakilishi wa miktadha mbalimbali ya jiografia na ya kijamii. DRC ilijumuishwa kwa sababu ni muktadha ulioathiriwa na mizozo, Guatemala kwa sababu inazingatia jamii za Asili na za mashambani, na Yordani kwa sababu ina idadi kubwa ya wakimbizi. Uanuai huu uliwezesha utafiti kuchunguza tofauti za mbinu za uwekaji muktadha na kutambua changamoto za kipekee katika maeneo mbalimbali.

## MASUALA YA MAADILI

Utafiti huu ulitii miongozo madhubiti ya kimaadili ili kulinda haki na faragha ya washiriki. Washiriki wote walitoa idhini baada ya kufahamishwa, na walipewa habari wazi kuhusu haki yao ya kujiondoa kwenye utafiti wakati wowote. Suala la kulinda usalama na faragha ya washiriki, hasa waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia, lilizingatiwa kwa upekee.

## KIAMBATISHO CHA 2

# Sauti za wateja

## KUANGAZIA DRC



Wateja wanalalamikia jinsi miradi ya kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia inavyowekewa muktadha, ijapokuwa uwajibikaji kwa watu walioathiriwa (AAP) unaendelea kuwa wito kwa wote wanaohusika katika juhudi za uhisani.

Nchini DRC, **matukio 46,000 ya unyanyasaji wa kingono yaliripotiwa katika mikoa** ya Kivu Kaskazini na Kusini na Ituri pekee kati ya Januari na Agosti 2023.[10] Wanawake na wasichana walialikwa kushiriki katika majadiliano ya vikundi kuhusu kama juhudi za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia zinawekewa muktadha ili kutimiza mahitaji yao na jinsi hili linavyofanywa. Muhtasari wa majadiliano hayo ya vikundi umetolewa hapo chini:

### USHIRIKI KATIKA UWEKAJI MUKTADHA

Wasichana katika jamii wenyeji waliripoti mafanikio na kuhusika zaidi katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, hasa katika mradi wa ufugaji wa kuku na wa kinyozi. Miradi hii ilitoa fursa za kuchuma kipato na iliwasaidia wasichana hao kukuza ujuzi wa kiutendaji. Kupitia mradi wa ufugaji wa kuku, wasichana wengi waliweza kuchuma mapato na kupata uhuru wa kifedha, jambo ambalo lilikuwa na athari chanya kwa kujiamini kwao. Vivyo hivyo, mradi wa kinyozi uliwapatia nafasi ya kuendesha biashara ndogo, na hivyo kuwawezesha zaidi na kuwapa hisia ya umiliki.

Kinyume na hayo, wasichana wanaoishi katika makambi walihisi kutelekezwa na kutowezeshwa. Licha ya kushiriki katika mipango ya uhamasishaji kama vile “Girl Shine” (Dada Ng’aa) na “Safe at Home” (Salama Nyumbani), walihisi kwamba mahitaji yao hayakushughulikiwa kikamilifu. Miradi katika kambi ilikuwa michache na mara nyingi ilipuuza mahitaji mahususi ya wasichana hao. Wasichana hao pia walieleza kutamaushwa na jinsi mkuu wa kambi anavyodhibiti uwezo wa kupata rasilimali na huduma, ambapo upendeleo ulichangia kuamua nani atapata usaidizi. Mfumo huu ulileta hisia za kutengwa na kutowezeshwa.

### VIZUIZI

**Matatizo ya usalama na usaidizi haba**

Wasichana katika jamii wenyeji walinufaika na miradi madhubuti zaidi iliyojumuisha uwezeshaji wa kiuchumi na ufahamishaji kuhusu unyanyasaji wa kijinsia. Hata hivyo, walitaja kwamba uzingatiaji wa utamaduni na ujumuishaji wa maoni ya eneo ni muhimu sana kwa mafanikio ya miradi hii.

Wasichana walio katika kambi walikabiliwa na hatari mbaya za kiusalama, hasa wakati wa kukusanya kuni. Wengi walieleza kutamaushwa na ugawaji wa maharage kutoka kwa mashirika ya uhisani, hali iliyowalazimu kwenda msituni kukusanya kuni ili kuyapika. Ziara hizi mara nyingi ziliwaweka katika hatari ya unyanyasaji wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na dhuluma za kingono na uonevu, hasa walipolazimika kwenda pweke. Msichana mmoja alieleza:

> ***“Ilibidi tutembee masafa marefu, wakati mwingine kwa siku kadhaa, kukusanya kuni za kupika maharage tuliyopewa. Tulikuwa peke yetu msituni na katika hatari ya kushambuliwa au kubakwa.”***

10 https://www.wfp.org/stories/eastern-drc-women-and-girls-pay-high-price-ongoing-conflict

## VIZUIZI

### Mahitaji yasiyotimizwa

Ijapokuwa wasichana katika jamii wenyeji walipokea fursa za kuzalisha mapato (kama vile ufugaji kuku na kinyozi), wale walio katika kambi walikuwa na fursa chache za kuwawezesha kiuchumi. Wasichana wengi walieleza shauku ya kuwepo kwa miradi zaidi mahususi ambayo ingewapa ujuzi wa biashara, ujasiriamali na rasilimali za kifedha.

Pengo muhimu lililotambuliwa na wasichana katika jamii wenyeji na pia walio katika kambi ni ukosefu wa huduma za afya ya akili. Wasichana wengi walitatizika na kiwewe cha kihisia na msongo wa kisaikolojia, hasa kutokana na unyanyasaji wa kijinsia, lakini miradi iliyopo haikushughulikia mahitaji yao ya afya ya akili kikamilifu.

## MAPENDEKEZO YA KUBORESHA HALI

» Ongeza uingatiaji wa maeneo salama na miundomsingi, kama vile mwangaza bora, sehemu zenye usalama kwa ajili ya wasichana na usafiri salama wa kufikia rasilimali.

» Wasichana katika jamii wenyeji na pia walio katika kambi walisisitiza hitaji la kuwepo kwa miradi inayozingatia utamaduni na kufaa muktadha. Katika jamii wenyeji, miradi inalingana na maadili na tamaduni za eneo, lakini hali haikuwa hivi kila wakati katika kambi, ambapo kulikuwa na vizuizi vya lugha na kutoelewana kwa misingi ya tamaduni. Wasichana walipendekeza kwamba miradi inafaa kutoholewa ili kushughulikia changamoto mahusisi zinazowakabili, ikiwa ni pamoja na usaidizi wa afya ya akili na fursa zaidi za kiuchumi zinazowalenga.

» Pendekezo lililojitokeza mara kwa mara kutoka kwa wasichana ni kujumuisha kina baba katika miradi ya familia. Ijapokuwa kina mama walihudhuria vikao mara kwa mara, kina baba hawakuhusika sana, licha ya wajibu muhimu wanaotekeleza katika kukuza mazingira bora kwa ajili ya wasichana. Ukosefu huu wa kuhusika kwa wanafamilia—hasa wa kiume—ulitajwa kama kizuizi cha usaidizi fanifu kwa usalama na ustawi wa wasichana.



*Picha imepigwa na* ***Daniel Ssemogerere*** *kwa ajili ya IRC*

## KUANGAZIA GUATEMALA



Guatemala ni mojawapo ya nchi zenye viwango vya juu zaidi vya mauaji ya wanawake duniani. Katika mwaka wa 2022, Lango la Takwimu la Shirika la Uangalizi wa Wanawake liliripoti **mauaji 534 ya wanawake**, na kufikia Machi 2023 matukio 69 ya mauaji ya wanawake yameripotiwa[11]. Majadiliano ya vikundi yalifanywa na wanawake wa Asili na vikundi vingine vilivyotengwa ili kuelewa jinsi miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia imetoholewa kutimiza mahitaji yao. Muhtasari wa majadiliano hayo ya vikundi umetolewa hapo chini:

### USHIRIKI KATIKA UWEKAJI MUKTADHA

Miradi iliwapatia wanawake hao maarifa muhimu kuhusu haki zao na aina za unyanyasaji ambazo huenda wakapitia. Washiriki walisisitiza jinsi mradi ulivyozingatia kuweka mahali salama kwa ajili ya wanawake na kutohoa maudhui kwa ajili ya mahitaji yao (kwa mfano, lugha na mwingiliano wa vikundi). Washiriki wengi walishiriki kwamba miradi hiyo iliwasaidia kuelewa haki zao na jinsi ya kupinga unyanyasaji katika jamii zao.

Kuwahusisha washiriki katika mchakato wa utohozi kulikuwa muhimu sana katika kuhakikisha ufikiaji wa mradi.

Washiriki walihusishwa kikamilifu katika kupendekeza mabadiliko katika mradi ili kuboresha ufikiaji wake. Walipendekeza mabadiliko ya ratiba, mahali na shughuli ili kuhakikisha wanawake wengi zaidi wangeweza kushiriki.

Wanawake wengi walieleza kuwa mradi huo ulitimiza mahitaji yao ya kihisia na pia ya hali halisi. Mifano ilikuwa pamoja na kupokea usaidizi wa kisheria na wa kisaikolojia, na kupata ujasiri wa kutetea haki zao.

Wanawake waliripoti kwamba mwendesha vipindi alikuwa mkarimu na alipokea maoni yao. Waliwasilisha mahitaji yao moja kwa moja kwa mwendesha vipindi na kutoa mapendekezo ya kuboresha mradi hata zaidi.

### VIZUIZI

Baadhi ya vizuizi vya kushiriki vilikuwa pamoja na ukosefu wa muda kutokana na majukumu ya nyumbani na changamoto za kiuchumi hasa katika usafiri. Zaidi ya hayo, baadhi ya wanawake walipata upinzani kutoka kwa wanafamilia kuhusiana na kushiriki kwao.

### MAPENDEKEZO YA KUBORESHA HALI

- Mapendekezo yalikuwa ni pamoja na haja ya usaidizi wa kiuchumi kwa ajili ya usafiri na vichocheo vya kushiriki, kuweka maeneo ya kukutana yanayofikiwa kwa urahisi zaidi, na mafunzo zaidi ya kukuza ujuzi wa kuwezesha.
- Washiriki walisisitiza umuhimu wa kufanya miradi iwe nyumbufu zaidi na ya kufaa utamaduni. Pia walieleza haja ya mafunzo zaidi ya kiufundi na rasilimali za kuhakikisha ushiriki zaidi.
- Washiriki pia waliangazia umuhimu wa mbinu za uwasilishaji ambazo zinazingatia utamaduni na ni nyumbufu ili kuhakikisha ushirikishi wenye mafanikio.

11 *https://openknowledge.worldbank.org/server/api/core/bitstreams/91b0eadb-e919-411c-8d19-329a8f17a325/content*

# KUANGAZIA YORDANI



Nchini Yordani, **asilimia 21 ya wanawake wanaripoti kunyanyaswa kimwili au kingono** na mpenzi katika maisha yao[12]. Majadiliano ya vikundi yalitathmini ni kwa kiasi kipi huduma za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia zinatimiza mahitaji ya vikundi mbalimbali vya watu, ikiwa ni pamoja na wakimbizi kutoka Siria na jamii wenyeji. Muhtasari wa majadiliano hayo ya vikundi umetolewa hapo chini:

## USHIRIKI KATIKA UWEKAJI MUKTADHA

Wasichana huko Yordani walieleza shauku kubwa ya kuwa na vipindi shirikishi vingi zaidi katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Walipendekeza kujumuisha uigizaji na maonyesho zaidi katika majadiliano kuhusu uonevu na unyanyasaji. Shughuli hizi ziliwasaidia kuhusika kwa undani na mada nyeti na kuelewa vyema zaidi haki zao na suala la unyanyasaji wa kijinsia.

Changamoto iliyojitokeza kila wakati kwa wasichana nchini Yordani ilikuwa wakati wa vipindi hivi. Wasichana wengi walipata ugumu kushiriki kwa sababu viligongana na ratiba za shule na vipindi vya mtihani. Walipendekeza kuweka muda unaweza kubadilishwa au kuweka vipindi hivyo siku za wikendi ili kuendana na ratiba zao za shule.

Wasichana hao pia walitaja umuhimu wa kujumuisha kina baba katika miradi ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Ijapokuwa kina mama walihusika mara nyingi, wasichana wengi walihisi kwamba kuhusika kwa kina baba ni muhimu sana katika kubadilisha kaida za kijinsia na kuleta mwingiliano jumuifu katika familia. Hata hivyo, wanafamilia wa kiume, hasa kina baba, mara nyingi walikataa kuhudhuria vipindi kama hivyo kwa sababu ya masuala ya kitamaduni.

## VIZUIZI

Nchini Yordani, masuala mengi ya kitamaduni yaliifanya vigumu kwa wasichana kuzungumza waziwazi kuhusu masuala kama vile uhalifu wa mtandaoni, unyanyasaji wa kingono na hedhi. Miiko inayohusiana na mada hizi ilimaanisha kwamba wasichana wengi walihisi kutohusika katika vipindi au walisita kuzungumza katika mazingira ya kikundi.

## MAPENDEKEZO YA KUBORESHA HALI

» Wasichana huko Yordani walipendekeza mbinu shirikishi zaidi kama vile uigizaji na majadiliano yanayowahusisha washiriki kuhusu matukio ya hali halisi. Walipendekeza pia kwamba vipindi hivi viratibiwe ili viingiane na ratiba zao za shule ambazo zina shughuli nyingi.

» Wasichana hao walipendekeza vipindi jumuifu zaidi vya familia, hasa kina baba wahudhurie, ili kukuza usawa wa jinsia na kuboresha uelewa wa masuala ya unyanyasaji wa kijinsia katika familia.

12 *https://dhsprogram.com/pubs/pdf/SR256/SR256.pdf*



**Uwekaji Muktadha katika Juhudi za Kuzuia na Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia: Maneno Tu au Hali Halisi kwa Mashirika Yanayoongozwa na Wanawake na ya Kutetea Haki za Wanawake katika Miktadha ya Uhisani?**

*International Rescue Committee*
*Desemba 2024*